



**MFUKO WA UDHAMINI WA KUMBUKUMBU YA MWALIMU JULIUS K. NYERERE
WANUFAIKA WA UFADHILI KWA MWAKA 2020/2021**

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutoa taarifa kwa umma kuwa wanafunzi sita (6) wamepata Udhamini (Scholarships) kuendelea na masomo ya elimu ya juu kwa mwaka 2020/21 chini ya Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere. Kati ya wanafunzi hao, wanne (4) wamechaguliwa kusoma Shahada ya Kwanza na wawili (2) Shahada ya Uzamili katika vyuo vikuu vilivyopo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa Shahada ya Kwanza, ufadhili umetolewa kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa Daraja la Kwanza ambao ni miongoni mwa wanafunzi 10 bora kitaifa waliomaliza kidato cha sita mwaka 2020. Kwa Shahada za Uzamili, ufadhili umetolewa kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika Shahada ya Kwanza.

Wanafunzi waliopata udhamini wa masomo ya Shahada ya Kwanza ni:

- 1. Bi. Maria Hewa GAMBALOYA**, atasomea fani ya **Sayansi -Uhandisi wa Umeme**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- 2. Bi. Marietha Pastory MONDEA**, atasomea fani ya **Sayansi- Uchambuzi Masuala ya Bima**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- 3. Bi. Nisha Ben-Nathan NKYA**, atasomea fani ya **Uhandisi wa Kompyuta na Teknologia ya Habari**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na
- 4. Bw. Alex Joseph MBOGO**, atasomea fani ya **Udaktari** katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Kwa Shahada ya Uzamili, wanafunzi waliopata ufadhili ni:

- 1. Bi. Monica MREMA**, atasoma Shahada ya **Sayansi Takwimu**, Chuo Kikuu cha Dodoma, na

2. Bw. Amour Kombo AME, atasoma Shahada ya **Uzamili ya Uchumi na Fedha** katika Chuo Kikuu cha Zanzibar.

Ufadhili unaotolewa chini ya Mfuko huu unajumuisha gharama zote za ada, pesa za kujikimu (malazi na chakula), mafunzo kwa vitendo na vifaa vya kujifunzia, ikiwemo kompyuta mpakato (Laptop).

Kwa maelezo zaidi kuhusu udhamini huo tembelea tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: www.bot.go.tz.

Tangazo hili limetolewa na:

Mwenyekiti, Kamati ya Mfuko wa Udhamini wa
Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere,
Benki Kuu ya Tanzania,
2 Mtaa wa Mirambo,
11884, DAR ES SALAAM.